# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA TISA

**22 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 22 APRILI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**106. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Wodi ya Upasuaji ya Wanawake na Jengo la kuhifadhia Maiti Hospitali ya Wilaya ya Karatu.

**107. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kutenga fedha za kujenga uzio katika Shule za Msingi na Sekondari - Temeke.

**108. MHESHIMIWA STANSLAUS SHING'OMA MABULA (NYAMAGANA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani kuiongezea fedha TARURA ili kujenga Barabara za ndani ikiwemo ya Mkuyuni - Mahina hadi Nyakato.

**109. MHESHIMIWA JONAS VAN ZEELAND (MVOMERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Daraja kuunganisha Kijiji cha Digoma na Digalama katika Mto Mjonga - Mvomero.

**WIZARA YA NISHATI:**

**110. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Vitongoji vyote vya Jimbo la Tarime Vijijini vitapata Umeme wa REA.

**WIZARA YA AFYA:**

**111. MHESHIMIWA AMINA ALI MZEE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini suala la Hedhi Salama litapewa kipaumbele kwa kugawa taulo za kike bure Shule za Msingi na Sekondari na kuboresha miundombinu ya Vyoo.

**WIZARA YA KILIMO:**

**112. MHESHIMIWA HASSAN SELEMAN MTENGA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaagiza Mazao ya Mbaazi na Ufuta kusafirishwa kupitia Bandari ya Mtwara.

**113. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhifadhi Mbegu na Mimea ya Asili kwa ajili ya vizazi vijavyo.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**114. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, nini mpango wa Serikali kujenga nyumba za Askari Polisi na Magereza eneo la Bangwe Kigoma Mjini.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**115. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini zoezi la ulinzi kwa Wavuvi wa Ziwa Tanganyika litaanza.

**WIZARA YA MAJI:**

**116. MHESHIMIWA SHANIF JAMAL MANSOOR (KWIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini fedha za kuboresha mtandao wa maji kutoka Mhalo - Ngudu katika Jimbo la Kwimba zitalipwa.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**117. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, zipi haki za Abiria wa Vyombo vya Moto nchini na kwa kiwango gani wanatambua haki zao.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**118. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kulinda haki za Watoto kwani kuna ongezeko kubwa la uvunjifu wa haki za Watoto nchini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **22 APRILI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA